# CHUKUA ITIKADI YAKO

# KUTOKA

# NDANI YA QUR'AN NA HADITHI SAHIHI

SHEIKH MUHAMMAD JAMIIL ZAINU

MKALIMANI: UMMATI ABDALLAH

IBNU UTHAIMIN ISLAMIC CENTRE, HAZINA DODOMA

17 RABI'UL AWWAL 1445 - 1 OCTOBER 2023

# KWA JINA LA ALLAH MWINGI WA REHMA

# MWENYE KUREHEMU

**Hakika sifa zote njema anastahiki Allah, tunamsifu na tunamuomba msamaha na tunajikinga kwa Allah kutokana na shari za nafsi zetu na ubaya wa matendo yetu. Yeyote ambaye ameongozwa na Allah hakuna wa kumpoteza na aliyempoteza hakuna wa kumuongoza.**

**Na ninashuhudia kwamba hapana muabudiwa wa haki isipokuwa Allah pekee hana mshirika na ninashuhudia kwamba hakika Muhammad ni mja wake na Mtume wake.**

**Ama baada ya utangulizi:**

**Haya ni maswali muhimu kuhusu Itikadi nimeyajibu pamoja na kutaja dalili kutoka ndani ya Qur'an na hadithi ili atulizane msomaji katika usahihi wa jawabu; kwa sababu itikadi ya upekee wa Allah ndio msingi wa mafanikio ya mwanadamu duniani na akhera.**

**Na ninamuomba Allah awanufaishe waislamu kwa risala hii na ajaalie utakasifu wa nia kwa ajili ya Allah.**

**Sheikh Muhammad Jamiil Zainuu**

# HAKI YA ALLAH JUU YA WAJA WAKE.

**SWALI LA KWANZA : Allah ametuumba kwa ajili ya kitu gani ?**

**JIBU: Ametuumba ili tumuabudu yeye wala tusimshirikishe na chochote. Na dalili juu ya hilo ni kauli yake Allah mtukufu ndani ya suratu Adhaariyaat: [ Na wala sikuwaumba majini nawanadamu isipokuwa waniabudu. ] Adhaariyaat 56.**

**Na kauli ya Mtume swallallaahu alaihi wasallam: [ Haki ya Allah iliyo juu ya waja wake ni wamuabudu yeye peke yake wala wasimshirikishe na chochote. ] Bukhari na Muslim.**

**SWALI LA PILI: Ni nini maana ya ibada?**

**JIBU: Ibada ni jina lenye kukusanya kila ambacho Allah anakipenda miongoni mwa maneno na vitendo, kama vile dua na swala na kuchinja na ibada nyinginezo. Amesema Allah mtukufu [ Sema hakika swala zangu na kuchinja kwangu na uhai wangu na kifo changu ni kwa ajili ya Allah Mola Mlezi wa ulimwengu…] Al-an'am 162.**

***Nusukiy: Ni kuchinja kwangu wanyama.**

**Na amesema Mtume swallallaahu alaihi waallam; [ Hatojisogeza kwangu mja wangu kwa kufanya jambo nilipendalo zaidi kuliko lile nililomfaradhishia ] Hadithi Qudsiy ameipokea Bukhari.**

**SWALI LA TATU: Namna gani tunamuabudu Allah?**

**JIBU: Kama alivyotuamrisha Allah na Mtume wake swallallaahu alaihi wasallam. Amesema Allah Mtukufu : [ Enyi mlioamini mtiini Allah na mtiini Mtume na wala msiharibu matendo yenu ] Muhammad 33.**

**Na amesema Mtume swallallaahu alaihi wasallam: [ Yeyote atakayefanya kitendo chochote cha ibada ambacho hakina amri yetu, basi kitarejeshwa ] yaani si chenye kukubaliwa. Ameipokea Muslim.**

**SWALI LA NNE: Je, tunamuabudu Allah kwa kumuogopa na kumtarajia?**

**JIBU: Ndiyo; tunamuabudu Allah katika hali hiyo. Amesema Allah Mtukufu akiwasifia waumini : [ wanamuomba Mola wao kwa kumuogopa na kumtarajia ] Assajdah 16**

**Na amesema Mtume swallallaahu alaihi wasallam ; [ Namuomba Allah pepo na najikinga**

**kwake kutokana na moto ]. Hadithi Sahihi imepokelewa na Abuu Daud.**

**SWALI LA TANO: Nini maana ya Ihsani katika ibada?**

**JIBU: Ihsani ni kuchunga uwepo wa Allah Mtukufu unapokuwa ndani ya ibada. Amesema Allah Mtukufu . [ Allah ambaye anakuona wakati usimamapo kuswali na unapogeukageuka miongoni mwa wenye kusujudu ] Ashu'araa 218-219.**

**Na amesema Mtume swallallaahu alaihi wasallam: [ Ihsani ni kumuabudu Allah kama vile unamuona; endapo humuoni basi hakika yeye anakuona.] Ameipokea Muslim.**

## AINA ZA UPEKEE WA ALLAH NA FAIDA ZAKE:

**SWALI LA SITA: Kwanini Allah alituma Mitume?**

**JIBU: Allah aliwatuma Mitume kwa ajili ya kutoa wito katika kumuabudu yeye peke yake na kumpingia ushirikina. Amesema Allah Mtukufu; [ Na hakika tulipeleka mtume katika kila umma ili aseme muabuduni Allah tu na jiepusheni na wanaoabudiwa kinyume na yeye ] An-nahl 36.**

*** Twaghuti: ni shetani anayetoa wito wa kuelekea katika kumuabudu asiyekuwa Allah. Na amesema Mtume swallallaahu alaihi wasallam: [ Mitume wote ni ndugu ………na dini yao ni moja ] Bukhari na Muslim.**

**SWALI LA SABA: Ni upi upekee wa Allah katika Ulezi?**

**JIBU: Ni upekee wake katika matendo yake kama vile kuumba na kusimamia viumbe na mengineyo. Amesema Allah Mtukufu; [ Sifa zote njema anastahiki Allah Mola mlezi wa ulimwengu]**

**Na amesema Mtume swallallaahu alaihi wasallam: [ Wewe ndiye Mola Mlezi wa mbingu na Ardhi ] Bukhari na Muslim.**

**SWALI LA NANE: Ni upi upekee wa Allah katika ibada?**

**JIBU: Ni kumpwekesha Allah katika ibada katika vile dua na kuchinja na kuweka nadhiri. Amesema Allah Mtukufu: [ Na muabudiwa wenu ni mmoja tu, hapana muabudiwa wa haki isipokuwa yeye mwingi wa rehma mwenye kurehemu] Albaqarah 163.**

**Na amesema Mtume swallallaahu alaihi wasallam: [ Liwe jambo la kwanza ambalo utawaita**

**watu katika hilo ni kushuhudia kwamba hapana muabudiwa wa haki isipokuwa Allah] na katika mapokezi ya Bukhari : [ ….. wampwekeshe Allah ]**

**SWALI LA TISA: Ni upi upekee wa Majina ya Allah na Sifa zake?**

**JIBU: Ni kuthibitisha ambacho Allah amejisifia yeye mwenyewe ndani ya kitabu chake , au ambacho amemsifia kwacho Mtume wake swallallaahu alaihi wasallam ndani ya hadithi sahihi, uthibitishaji wa maana ya hakika , bila ya kugeuza maana wala kuegemeza maana, wala kufananisha, wala kupinga. Kama vile sifa ya "Kuwa juu ya Arshi" na 'Kuteremka' na 'Mkono' na sifa nyinginezo ambazo zinaendana na ukamilifu wake.**

**Amesema Allah Mtukufu: [ Hakuna chochote mfano wake, naye ni msikivu na mwenye kuona ] Ashuuraa 11. Na amesema Mtume swallallaahu alaihi wasallam: [ Anateremka Allah kila usiku mpaka katika mbingu ya dunia] Ameipokea Muslim.**

***Anateremka uteremkaji ambao unaendana na utukufu wake, haufanani na uteremkaji wa yeyote miongoni mwa viumbe wake.**

**SWALI LA KUMI: Yupo wapi Allah?**

**JIBU: Allah yupo juu ya Arshi, juu ya mbingu. Amesema Allah Mtukufu: [ Allah mwingi wa rehma yupo juu ya arshi amestawi ] Twaaha 5. Yaani yupo juu. Kama ilivyokuja ndani ya Bukhari . Na amesema Mtume swallallaahu alaihi wasallam : [ Hakika Allah aliandika kitabu… kitabu hicho kipo kwake juu ya arshi ] Bukhari na Muslim.**

**SWALI LA KUMI NA MOJA: Je, Allah yupo pamoja na sisi?**

**JIBU: Allah yupo pamoja na sisi kwa kusikia kwake na kuona kwake na elimu yake. Amesema Allah Mtukufu: [ Allah akasema, msiogope hakika mimi nipo pamoja na ninyi ninasikia na ninaona] Twaaha 46.**

**Na amesema Mtume swallallaahu alaihi wasallam: [ Hakika ninyi mnamuomba Allah mwenye kusikia na yupo karibu, naye yupo pamoja nanyi ] Ameipokea Muslim**

***Yaani yupo pamoja nanyi kwa elimu yake.**

**SWALI LA KUMI NA MBILI: Ni ipi faida ya kumpwekesha Allah (Tauhidi)?**

**JIBU: Faida ya kumpwekesha Allah (Tauhidi) ni kupata amani akhera dhidi ya adhabu na kupata mwongozo duniani na kufutiwa madhambi. Amesema Allah Mtukufu: [ Wale ambao wameamini na wala hawakuchanganya imani yao na ushirikina hao ndio wenye amani nao ndio wenye kuongoka ] Al-an'am 86.**

**Na amesema Mtume swallallaahu alaihi wasallam: [ Haki ya waja kwa Allah ni kutoadhibiwa yule ambaye hakumshirikisha Allah na chochote] Bukhari na Muslim.**

## MASHARTI YA KUKUBALIKA MATENDO:

**SWALI LA KUMI NA TATU: Ni yepi masharti ya kukubalika matendo?**

**JIBU: Masharti ya kukubalika matendo mbele ya Allah ni matatu:-**

1) **Kumuamini Allah na kumpwekesha. Amesema Allah Mtukufu: [ Hakika wale walioamini na wakafanya matendo mema yatakuwa mabustani ya firdausi ndio mafikio yao ] Alkahf 108. Na amesema Mtume swallallaahu alaihi wasallam : [ Sema nimemuamini Allah kisha kuwa na msimamo ] Ameipokea Muslim.**
2) **Kutakasa nia. Nako ni kutenda kwa ajili ya Allah bila ya kujionyesha wala kutaka kusikika. Amesema Allah Mtukufu: [ wamuabudu Allah katika hali ya kumtakasia matendo] Al-bayyinah 5.**
3) **Kuafikiana na yale ambayo amekuja nayo Mtume swallallaahu alaihi wasallam. Amesema Allah Mtukufu: [ Na yale ambayo amekupeni Mtume yachukueni na yale ambayo amekukatazeni basi yaacheni ] Al-hashr 7. Na amesema Mtume swallallaahu alaihi wasallam: [ Yeyote atakayefanya tendo lolote la kiibada ambalo halina amri yetu, basi litarejeshwa. ] yaani litakataliwa. Ameipokea Muslim**

## USHIRIKINA MKUBWA.

**SWALI LA KUMI NA NNE: Ni ipi dhambi kubwa zaidi mbele ya Allah?**

**JIBU: Dhambi kubwa zaidi mbele ya Allah ni kumshirikisha Allah. Na dalili ni kauli yake Allah: [ Ewe mwanangu usimshirikishe Allah, hakika ushirikina ni dhulma iliyokuwa kubwa zaidi ] Luqmaan13 . Na pindi alipoulizwa Mtume swallallaahu alaihi wasallam: [ Ni dhambi ipi kubwa zaidi? Akasema : 'Ni kumfanyia Allah mwenza hali ya kuwa Allah ndiye amekuumba ] Bukhari na Muslim. Mwenza ni mshirika.**

**SWALI LA KUMI NA TANO: Ni upi ushirikina mkubwa?**

**JIBU: Ushirikina mkubwa ni kuelekeza ibada kwa asiyekuwa Allah, kama vile kumuomba asiyekuwa Allah, na kuomba ulinzi kwa waliokufa au waliohai wasiokuwepo. Amesema Allah Mtukufu: [ Na muabuduni Allah wala msimshirikishe na chochote] Annisaa 36. Na amesema Mtume swallallaahu alaihi wasallam: [ Dhambi iliyokubwa zaidi ni Kumshirikisha Allah] Ameipokea Bukhari.**

**SWALI LA KUMI NA SITA: Je, ushirikina upo katika umma huu?**

**JIBU: Ndiyo upo; na dalili ni kauli yake Allah Mtukufu : [ Na wengi wao hawatomwamini Allah isipokuwa nao ni washirikina ] Yuusuf 106. Na amesema Mtume swallallaahu alaihi wasallam [ Hakitosimama Qiyama mpaka makabila katika umma wangu yaungane na washirikina na mpaka yaabudu masanamu ] Hadithi sahihi ameipokea Attirmidhiy .**

**SWALI LA KUMI NA SABA: Ni ipi hukumu ya kuwaomba waliokufa au wasiokuwepo?**

**JIBU: Kuwaomba waliokufa au wasiokuwepo ni miongoni mwa ushirikina mkubwa. Amesema Allah Mtukufu: [ Wala usimuombe kinyume na Allah yeyote ambaye hawezi kukunufaisha wala kukudhuru, endapo utafanya hivyo basi hakika wewe utakuwa miongoni mwa madhalimu] yaani washirikina. Yuunus 106.**

**Na amesema Mtume swallallaahu alaihi wasallam [ Yeyote atakayekufa hali ya kuwa anamuomba mwenza kinyume na Allah pekee basi ataingia motoni ] Ameipokea Bukhari.**

**SWALI LA KUMI NA NANE: Je, dua ni ibada?**

**JIBU: Ndiyo; Dua ni ibada. Amesema Allah Mtukufu: [ Na amesema Mola wenu Mlezi niombeni mimi nitakujibuni, hakika wale ambao wanafanya kiburi katika ibada yangu watangia ndani ya moto wa Jahannam kwa udhalili ] Ghaafir 60. Na amesema Mtume swallallaahu alaihi wasallam: [ Dua ndio ibada ] ameipokea Ahmad na amesema Attirmidhiy hadithi Hasan na Sahihi.**

**SWALI LA KUMI NA TISA: Je, waliokufa wanasikia maombi?**

**JIBU: Hawasikii; amesema Allah Mtukufu: [ Hakika wewe huwezi kuwasikilizisha waliokufa ] Annaml 80. [ Na hakika wewe huwezi kuwasikilizisha waliomo makaburini ] Faatir 22.**

**AINA ZA USHIRIKINA MKUBWA:**

**SWALI LA ISHIRINI: Je, tuombe kuokolewa na waliokufa au wasiokuwepo?**

**JIBU: Tusiombe kuokolewa na waliokufa wala wasiokuwepo. Amesema Allah Mtukufu: [ Na wale ambao wanawaomba kinyume na Allah hawawezi kuumba chochote bali wao wameumbwa : Wamekufa hawako hai, na wala hawajui lini watafufuliwa] Annaml 20-21. Na amesema Allah mwenye nguvu na aliyetukuka: [ Pindi mnapomuomba mola wenu akuokoeni kisha anakujibuni ] Al-anfaal 9.**

**Na amesema Mtume swallallaahu alaihi wasallam : [ Ewe uliye hai na msimamizi, kwa rehma zako naomba uniokoe] Hadithi Hassan ameipokea Attirmidhiy.**

**SWALI LA ISHIRINI NA MOJA: Je, inafaa kuomba msaada kwa asiyekuwa Allah?**

**JIBU: Haifai, na dalili ni kauli yake Allah Mtukufu: [ Wewe tu ndiye tunakuabudu na wewe tu ndiye tunakuomba msaada ] Alfaatiha 5; na kauli yake Mtume swallallaahu alaihi wasallam: [ Pindi unapoomba basi muombe Allah, na pindi unapoomba msaada basi muombe msaada Allah ] Hadithi Hassan na Sahihi ameipokea Attirmidhiy.**

**SWALI LA ISHIRINI NA MBILI: Je, tuombe msaada kwa waliohai?**

**JIBU: Ndiyo, katika jambo ambalo wanaliweza. Amesema Allah Mtukufu: [ Na saidianeni katika wema na uchamungu ] Almaaidah 2.**

**Na amesema Mtume swallallaahu alaihi wasallam: [ Na Allah yupo katika kumsaidia mja pindi mja atakapokuwa katika kumsaidia ndugu yake] Ameipokea Muslim.**

**SWALI LA ISHIRINI NA TATU: Je, inafaa kuweka nadhiri kwa ajili ya asiyekuwa Allah?**

**JIBU: Haifai kuweka nadhiri isipokuwa kwa ajili ya Allah pekee, kwa kuli yake Allah Mtukufu: [ Ewe Mola wangu mlezi hakika mimi nimeweka nadhiri kwa ajili yako mtoto aliye tumboni kwangu akutumikie wewe ] Aal Imraan 35.**

**Na kauli yake Mtume swallallaahu alaihi wasallam: [ Yeyote aliyeweka nadhiri ya kumtii Allah basi amtii, na yeyote aliyeweka nadhiri ya kumuasi Allah, basi asimuasi ] Ameipokea bukhari.**

**SWALI LA ISHIRINI NA NNE: Je, inafaa kuchinja kwa ajili ya asiyekuwa Allah?**

**JIBU: Haifai, na dalili ni kauli yake Allah Mtukufu [ Swali kwa ajili ya Mola wako mlezi na uchinje kwa ajili ya Mola wako Mlezi ] Alkauthar 2. Na amesema Mtume swallallaahu alaihi wasallam: [ Amemlaani Allah yeyote mwenye kuchinja kwa ajili ya asiyekuwa Allah ] Ameipokea Muslim.**

**SWALI LA ISHIRINI NA TANO:Je, tuzunguke makaburi kwa ajili ya kujisogeza kwayo?**

**JIBU: Hatutajkiwi kuzunguka isipokuwa Alqaaba; amesema Allah Mtukufu : [ Na waizunguke nyumba kongwe ] Alhajj 29.**

**Na amesema Mtume swallallaahu alaihi wasallam: [ Yeyote atakayezunguka Alqaaba mara saba na akaswali rakaa mbili, malipo yake yanakuwa mfano wa kuacha huru mtumwa ] Hadithi sahihi ameipokea Ibnu Maajah.**

**SWALI LA ISHIRINI NA SITA: Ni ipi hukumu ya uchawi?**

**JIBU: Uchawi ni ukafiri. Amesema Allah Mtukufu: [ Lakini mashetani ndio waliokufuru wanawafundisha watu uchawi ] Albaqarah 102.**

**Na amesema Mtume swallallaahu alaihi wasallam: [ Jiepusheni na madhambi saba yenye kuangamiza: Kumshirikisha Allah na Uchawi…..] Ameipokea Muslim.**

**SWALI LA ISHIRINI NA SABA: Je, tunawaamini wapiga ramli na makuhani katika kuelezea elimu ya yaliyofichikana?**

**JIBU: Hatuwaamini, kwa kauli yake Allah Mtukufu : [ Sema hakuna yeyote mbinguni na ardhini mwenye kufahamu yaliyofichikana isipokuwa Allah ] Hadithi sahihi ameipokea Ahmad.**

**SWALI LA ISHIRINI NA NANE: Je, kuna kiumbe yeyote anafahamu yaliyofichikana?**

**JIBU: Hakuna kiumbe yeyote mwenye kufahamu yaliyofichikana isipokuwa yule ambaye ameonyeshwa na Allah katika mitume. Amesema Allah Mtukufu: [ Allah ndiye mjuzi wa yaliyofichikana hamuonyeshi yeyote katika elimu yake ya yaliyofichikana * Isipokuwa ambaye Allah amemridhia miongoni mwa mitume ] Al-jinn 26-27**

**Na amesema Mtume swallallaahu alaihi wasallam: [ Hakuna yeyote mwenye kufahamu yaliyofichikana isipokuwa Allah ] Hadithi Hasan,ameipokea Attwabaraaniy.**

### SWALI LA ISHIRINI NA TISA: Je, tuvae uzi na Kamba kwa ajili ya tiba?

**JIBU: Hatuvai, kwa sababu ya kauli yake Allah Mtukufu: [ Na endapo utapatwa na madhara basi hakuna yeyote wa kuyaondoa isipokuwa yeye Allah ] Al-an'am 17.**

**Na kauli yake Mtume swallallaahu alaihi wasallam: [ Hakika hiyo Kamba uliyoivaa haikuzidishii isipokuwa madhara, ivue ! hakika lau ungekufa katika hali hiyo usingefaulu kamwe ] Hadithi Sahihi ameipokea Haakim na ameisahihisha na amemuafiki Adhahabiy.**

### SWALI LA THELATHINI: Je, tutundike shanga na kaure na mfano wake?

**JIBU: Hatutakiwi kutundika kwa lengo la kuepukana na athari za kijicho. Kwa kauli yake Allah Mtukufu [ Na endapo endapo Allah atakupatia madhara basi hakuna yeyote wa kuyaondoa isipokuwa yeye Allah ] Al-an'am 17.**

**Na kauli ya Mtume swallallaahu alaihi wasallam: [ Yeyote atakayetundika hirizi hakika amefanya ushirikina ] Hadithi sahihi ameipokea Ahmad .**

*** Tamima: ni Shanga au kaure hutundikwa kwa lengo la kuepukana na athari za kijicho.**

### SWALI LA THELATHINI NA MOJA: Ni ipi hukumu ya kufanyia kazi kanuni zenye kupingana na Uislamu?

**JIBU: Kufanyia kazi kanuni zenye kupingana na uislamu ni ukafiri pindi atakapozipitisha au akaamini ufaaji wake. Amesema Allah Mtukufu: [ Na yeyote ambaye hatohukumu kwa kile ambacho amekiteremsha Allah basi hao ndio makafiri ] Al-maaidah 44.**

**Na amesema Mtume swallallaahu alaihi wasallam: [ Na watawala wao hawatohukumu kwa kutumia kitabu cha Allah, na wakachagua baadhi ya aliyoyateremsha Allah, isipokuwa Allah atajaalia uadui baina yao ] Hadithi Hasan ameipokea Ibnu Maajah na wengineo.**

**SWALI LA THELATHINI NA MBILI: Namna gani tutalipinga swali la shetani 'nani kamuumba Allah ' ?**

**JIBU: Pindi shetani atakapomshawishi mmojawenu kwa swali hili basi aombe ulinzi kwa Allah . Amesema Allah Mtukufu: [ Na endapo utakupata uchochezi kutoka kwa shetani basi omba ulinzi kwa Allah; hakika yeye ni msikivu na mjuzi ] Fuswilat 36.**

**Na Mtume swallallaahu alaihi wasallam ametufundisha tuzuie vitimbi vya shetani na tuseme; ' Nimemuamini Allah na Mtume wake ' [ Sema yeye Allah ni mmoja * Allah ndiye mkusudiwa wa haja * Hakuzaa wala hakuzaliwa * Na wala hakuna yeyote mfano wake ] Ikhlaas 1-4. Kisha ateme mate upande wa kushotoni kwake mara tatu, na aombe ulinzi kwa Allah dhidi ya shetani, kisha aache kufikiria swali hilo. Hakika mambo hayo yatamuondolea hali hiyo. Huu ni ufupisho wa hadithi sahihi zilizopokelewa ndani ya kitabu cha Bukhari na Muslim na Ahmad na Abuu Daud.**

**SWALI LA THELATHINI NA TATU: Je, ushirikina mkubwa unasababisha kukaa milele motoni?**

**JIBU: Ushirikina mkubwa unasababisha kukaa milele motoni. Amesema Allah Mtukufu: [ Hakika yeyote atakayemshirikisha Allah , hakika Allah amemharamishia juu yake pepo na mafikio yake ni motoni, na washirikina hawana wa kuwanusuru ] Al-maaidah 72.**

**Na amesema Mtume swallallaahu alaihi wasallam: [ Yeyote atakayekutana na Allah akiwa anamshirikisha ataingia motoni ] Ameipokea Muslim.**

**SWALI LA THELATHINI NA NNE: Je, matendo mema yatamnufaisha mtu akiwa pamoja na ushirikina?**

**JIBU: Matendo mema hayatomnufaisha mtu akiwa pamoja na ushirikina, kwa kauli yake Allah Mtukufu kuhusu mitume; [ Na lau kama mitume wangemshirikisha Allah yangeporomoka matendo mema waliyokuwa wakiyafanya ] Al-an'am 88.**

**Na Amesema Mtume swallallaahu alaihi wasallam: [ Amesema Allah aliyetukuka na aliyejuu: Hakika mimi si muhitaji wa washirika kunako kunishirikisha nao, yeyote atakayetenda kitendo akamshirikisha ndani yake mwingine pamoja nami, basi nitamuacha na mshirika wake ] Ameipokea Muslim.**

**USHIRIKINA MDOGO:**

**SWALI LA THELATHINI NA TANO: Ni upi ushirikina mdogo?**

**JIBU: Ushirikina mdogo ni ria (kujionyesha katika ibada). Amesema Allah Mtukufu: [ Yeyote anayetarajia kukutana na Mola wake, basi atende matendo mema na wala asimshirikishe yeyote katika kumuabudu Mola wake ] Alkahf 110.**

**Na amesema Mtume swallallaahu alaihi wasallam: [ Hakika jambo lenye kuhofisha zaidi ambalo nalihofia juu yenu ni ushirikina mdogo; ushirikina mdogo ni ria (kujionyesha katika ibada) ] Hadithi sahihi ameipokea Ahmad.**

**Na miongoni mwa ushirikina mdogo ni kauli ya mtu : [ lau kama si Allah na fulani… au akipenda Allah na ukipenda wewe.. ] Na akasema Mtume swallallaahu alaihi wasallam: [ Msiseme: 'Akipenda Allah na akipenda fulani' lakini semeni; 'Akipenda Allah kisha akipenda fulani' ] Hadithi sahihi ameipokea Abuu Daud.**

**SWALI LA THELATHINI NA SITA: Je, inafaa kuapa kwa kutumia jina la asiyekuwa Allah?**

**JIBU: Haifai kuapa kwa kutumia jina la asiyekuwa Allah. Amesema Allah Mtukufu: [ Sema ndivyo ilivyo naapa kwa jina la Mola wangu hakika mtafufuliwa ] Attaghaabun 7.**

**Na amesema Mtume swallallaahu alaihi wasallam: [ Yeyote atakayeapa kwa kutumia jina la asiyekuwa Allah, hakika amefanya ushirikina ] Hadithi sahihi ameipokea Ahmad. Na amesema Mtume swallallaahu alaihi wasallam: [ Yeyote atayekuwa anaapa basi aape kwa kutumia jina la Allah au anyamaze ] Bukhari na Muslim.**

**KUPITISHA MAOMBI NA KUTAFUTA UOMBEZI:**

**SWALI LA THELATHINI NA SABA: Tunapitisha maombi yetu kwa Allah kwa kutumia kitu gani?**

**JIBU: Upitishaji wa maombi kwenda kwa Allah ufaao na utakiwao ni kwa kutumia majina ya Allah na sifa zake na matendo mema. Amesema Allah Mtukufu: [ Na Allah anayo majina mazuri basi muombeni kwa kupitia majina hayo ] Al-a'raaf 180.**

**Na amesema Allah Mtukufu: [ Enyi mlioamini mcheni Allah na tafuteni kwake wasila ] Almaaidah 35. Yaani, Jisogezeni kwake yeye kwa kumtii na kufanya matendo yenye kumridhisha. Ameyataja maelezo haya Ibnu Kathiir akinukuu kutoka kwa Qataadah.**

**Na amesema Mtume swallallaahu alaihi wasallam: [ Ninakuomba kwa kutumia kila jina ambalo ni lako ] Hadithi sahihi imepokelewa na Ahmad.**

**Na kauli yake Mtume swallallaahu alaihi wasallam kwa swahaba ambaye alimuomba kuwa pamoja naye peponi: [ Nisaidie juu ya nafsi yako kwa kukithirisha kusujudu ] Yaani swala; nayo ni miongoni mwa matendo mema . Ameipokea Muslim.**

**Na inafaa kupitishia maombi yetu katika mapenzi yetu ya kumpenda Allah na Mtume wake swallallaahu alaihi wasallam na kuwapenda mawalii wa Allah. Kama vile katika kisa cha watu wa pangoni ambao walipitishia maombi yao katika matendo yao mema, Allah akawaondolea tatizo lao.**

## UPITISHAJI WA MAOMBI UNAOKATAZWA:

**Nao ni kuwaomba waliokufa na kuomba haja mbalimbali kutoka kwao, kama vile hali halisi ilivyo leo hii; nao ni ushirikina mkubwa kwa kauli yake Allah Mtukufu: [ Wala usimuombe kinyume na Allah yeyote ambaye hawezi kukunufaisha wala kukudhuru, ikiwa utafanya hivyo basi hakika wewe utakuwa miongoni mwa washirikina ] Yunus 106**

**Ama kupitishia maombi katika cheo cha Mtume swallallaahu alaihi wasallam; mfano kauli yako ; "Ewe Allah kupitia cheo cha Mtume naomba uniponyeshe" , hakika huo ni uzushi, kwa sababu maswahaba hawakufanya hivyo. Na sababu nyingine ni kwamba Umar Allah amridhie alipitishia maombi yake kwa Abbaas Allah amridhie alipokuwa hai na wala hakupitishia maombi yake kwa Mtume swallallaahu alaihi wasallam baada ya kifo chake. Na hakika upitishaji huu wa maombi unaweza kupelekea katika ushirikina; inakuwa hivyo pindi atakapoamini kwamba hakika Allah anahitaji uwakilishi wa mwanadamu kama vile kiongozi au mtawala , kwa sababu kamfananisha muumba na kiumbe.**

**Na ili kufahamu ziada ya ufafanuzi na dalili kuhusiana na maudhui hii itarejewa risala iitwayo { Kupitisha maombi na Hukumu zake na aina zake } ya sheikh Albaaniy.**

## SWALI LA THELATHINI NA NANE: Je, Dua inahitaji uwakilishi wa mwanadamu yeyote?

**JIBU: Dua haihitaji uwakilishi wa mwanadamu yeyote, kwa kauli yake Allah Mtukufu: [ Na pindi watakapokuuliza waja wangu kuhusu mimi waambuie hakika mimi nipo karibu ] Albaqarah 186.**

**Na kauli yake Mtume swallallaahu alaihi wasallam: [ Hakika ninyi mnamuomba Allah mwenye kusikia na aliye karibu , naye yupo pamoja nanyi ] Yaani, yupo pamoja nanyi kwa elimu yake.**

**SWALI LA THELATHINI NA TISA: Je, inafaa kuhitaji kuombewa dua na aliye hai?**

**JIBU: Inafaa kuhitaji kuombewa dua na aliyehai si aliyekufa; amesema Allah Mtukufu akimsemesha Mtume swallallaahu alaihi wasallam wakati akiwa hai: [ Na omba msamaha wa madhambi yako na madhambi ya waumini wa kiume na waumini wa kike ] Muhammad 19.**

**Na ndani ya hadithi sahihi ambayo ameipokea Attirmidhiy: [ Hakika mtu mmoja mwenye upofu wa macho alikwenda kwa Mtume swalllallahu alaihi wasallam akasema; " Ewe Mtume wa Allah niombee kwa Allah aniponyeshe" ]**

**SWALI LA AROBAINI: Ni upi uwakilishi wa Mtume swallallaahu alaihi wasallam?**

**JIBU: Uwakilishi wa Mtume swallallaahu alaihi wasallam ni kufikisha ujumbe wa Allah. Amesema Allah Mtukufu: [ Ewe Mtume fikisha kile ambacho kimeteremshwa kwako ] Al-maaidah 67.**

**Na akasema Mtume swallallaahu alaihi wasallam: [ Ewe Allah shuhudia] akijibu kauli ya swahaba aliposema; " Tunasuhudia hakika wewe umefikisha ujumbe" ] Ameipokea Muslim.**

**SWALI LA AROBAINI NA MOJA: Kwa nani tutafute uombezi wa Mtume swallallaahu alaihi wasallam?**

**JIBU: Tunatafuta uombezi wa Mtume swallallaahu alaihi wasallam kwa Allah. Amesema Allah Mtukufu: [ Sema uombezi wote unamilikiwa na Allah ] Azzumar 44.**

**Na mtume swallallaahu alaihi wasallam alimfundisha swahaba mmoja aseme : [ Ewe Allah nakuomba uombezi wa mtume kwangu mimi ] Hadithi Hasana na Sahihi ameipokea Attir-midhiy.**

**Na amesema Mtume swallallaahu alaihi wasallam: [ Hakika mimi nimeficha maombi yangu kwa ajili ya kuwaombea umma wangu siku ya Qiyama kwa yule ambaye atakufa katika umma wangu akiwa hajamshirikisha Allah na chochote ] Ameipokea Muslim.**

**SWALI LA AROBAINI NA MOJA: Je, tuhitajie uombezi kutoka kwa waliohai?**

**JIBU: Tunahitajia uombezi kutoka kwa waliohai katika mambo ya kidunia. Amesema Allah Mtukufu: [ Yeyote atakayefanya uombezi mzuri atapata fungu katika uombezi huo, na yeyote atakayefanya uombezi mbaya atapata fungu katika uombezi huo ] Annisaa 85 Yaani**

**atapata fungu kutokana na madhambi ya uombezi huo mbaya.**

**Na amesema Mtume swallallaahu alaihi wasallam: [ Fanyeni uombezi mzuri mtalipwa thawabu ] Hadithi sahihi ameipokea Abuu Daud.**

## SWALI LA AROBAINI NA TATU: Je, tuzidishe katika kumsifu Mtume swallallaahu alaihi wasallam?

**JIBU: Hatutakiwi kuzidisha katika kumsifu Mtume swallallaahu alaihi wasallam. Amesema Allah Mtukufu: [ Sema hakika mimi ni mwanadamu mfano wenu, imefunuliwa kwangu kwamba muabudiwa wenu ni muabudiwa mmoja tu ] Al-kahf 110.**

**Na amesema Mtume swallallaahu alaihi wasallam: [ Msizidishe katika kunisifu kama ambavyo walivyozidisha manasara kumsifu Isa mtoto wa Maryam; hakika mimi ni mja wa Allah , basi semeni 'mja wa Allah na mtume wake' ] Ameipokea Bukhari.**

## JIHADI NA MAPENZI KWA AJILI YA ALLAH NA KUHUKUMU:

## SWALI LA AROBAINI NA NNE: Ni ipi hukumu ya jihadi katika njia ya Allah?

**JIBU: Jihadi ni wajibu kwa kutumia mali na nafsi na ulimi. Amesema Allah Mtukufu: [ Nendeni katika jihadi katika wepesi na uzito na fanyeni jihadi kwa mali zenu na nafsi zenu katika njia ya Allah ] Attaubah 4.**

**Na amesema Mtume swallallaahu alaihi wasallam: [ Wafanyieni jihadi washirikina kwa mali zenu na nafsi zenu na ndimi zenu ] Hadithi sahihi ameipokea Abuu Daud.**

## SWALI LA AROBAINI NA TANO: Ni yepi mapenzi kwa ajili ya Allah?

**JIBU: Ni kupendana na kunusuriana kwa ajili ya Allah. Amesema Allah Mtukufu: [ Na waumini wa kiume na waumini wa kike wanapendana wao kwa wao ] Attaubah 71.**

**Na amesema Mtume swallallaahu alaihi wasallam: [ Muumini kwa muumini mwenzake ni mfano wa jengo moja ambalo limeshikana na kuungana ] Ameipokea Muslim.**

**SWALI LA AROBAINI NA SITA: Je, inafaa kuwapenda makafiri na kuwanusuru?**

**JIBU: Haifai kuwapenda makafiri na kuwanusuru. Amesema Allah Mtukufu: [ Na yeyote atakayewapenda makafiri basi naye ni miongoni mwao ] Al-maaidah 51.**

**Na amesema Mtume swallallaahu alaihi wasallam: [ Hakina watu wa ukoo fulani si vipenzi vyangu ] Hadithi sahihi ameipokea Ahmad.**

**SWALI LA AROBAINI NA SABA: Ni nani walii?**

**JIBU: Walii ni muumini mchamungu. Amesema Allah Mtukufu: [ Zindukeni ! Hakika mawalii wa Allah hawatokuwa na hofu wala hawatohuzunika * Ni wale walioamini na wakawa wachamungu ]**

**Na amesema Mtume swallallaahu alaihi wasallam: [ Hakika kipenzi changu ni Allah na waumini wema ] Hadithi sahihi ameipokea Ahmad.**

**SWALI LA AROBAINI NA NANE: Waislamu wanahukumu kwa kutumia nini?**

**JIBU: Waislamu wanahukumu kwa kutumia Qur'an na hadithi sahihi. Amesema Allah Mtukufu: [ Na hukumu baina yao kwa kutumia kile ambacho amekiteremsha Allah ] Al-maaidah 49.**

**Na amesema Mtume swallallaahu alaihi wasallam: [ Mjuzi wa yaliyofichikana na yaliyowazi wewe ndiye unahukumu baina ya waja wako ] Ameipokea Muslim.**

**KUFANYIA KAZI QUR'AN NA HADITHI.**

**SWALI LA AROBAINI NA TISA: Kwa nini ameteremsha Allah Qur'an?**

**JIBU: Ameteremsha Allah Qur'an kwa ajili ya kuifanyia kazi. Amesema Allah Mtukufu : [ Fuateni yale ambayo mmeteremshiwa kutoka kwa Mola wenu ] Al-a'raaf 3.**

**Na amesema Mtume swallallaahu alaihi wasallam: [ Isomeni Qur'an na ifanyieni kazi, wala msile kwa ajili yake ] Hadithi sahihi ameipokea Ahmad.**

**SWALI LA KHAMSINI: Ni ipi hukumu ya kufanyia kazi hadithi sahihi?**

**JIBU: Kufanyia kazi hadithi sahihi ni wajibu, kwa kauli yake Allah Mtukufu: [ Na ambayo**

**amekupeni mtume yachukueni na ambayo amekukatazeni yaacheni ] Al-hashri 7.**

**Na amesema Mtume swallallaahu alaihi wasallam: [ Ni juu yenu kushikamana na sunna zangu na sunna za makhalifa wangu waongofu wenye kuongoza, shikamaneni nazo ] Hadithi sahihi ameipokea Ahmad.**

**SWALI LA KHAMSINI NA MOJA: Je, tunatosheka na Qur'an kwa kutohitajia hadithi?**

**JIBU: Hatotosheki na Qur'an kwa kutohitajia hadithi, amesema Allah Mtukufu: [ Na tumekuteremshia hadithi ili uwabainishie watu kile ambacho wameteremshiwa (Qur'an) ] Annahl 44.**

**Na amesema Mtume swallallaahu alaihi wasallam: [ Tambueni ! Hakika mimi nimepewa Qur'an na nimepewa pamoja na Qur'an mfano wake ] Hadithi sahihi ameipokea Abuu Daud na wengineo.**

**SWALI LA KHAMSINI NA MBILI: Je, tutangulize kauli ya mtu yeyote juu ya kauli ya Allah na Mtume wake swallallaahu alaihi wasallam?**

**JIBU: Hatutakiwi kutanguliza kauli ya mtu yeyote juu ya kauli ya Allah na Mtume wake swallallaahu alaihi wasallam , kwa kauli yake Allah Mtukufu: [ Enyi mlioamini msitanguilze chochote mbele ya kauli ya Allah na Mtume wake ] Al-hujuraat 1**

**Na amesema Mtume swallallahu alaihi wasallam: [ Hakuna kumtii kiumbe katika kumuasi muumba ] Hadithi sahihi ameipokea Attwabaraaniy.**

**Na kauli ya Ibnu Abbaas Allah amridhie: [ Naogopea mtashushiwa juu yenu mawe kutoka mbinguni ! Mimi nasema : 'amesema Mtume swallalllahu alaihi wasallam"; nanyi mnasema: 'Amesema Abuu Bakar na Umar ]**

**SWALI LA KHAMSINI NA TATU: Nini tufanye pindi tutakapotofautiana?**

**JIBU: Tunarejea katika kitabu cha Allah na Sunna sahihi . Amesema Allah Mtukufu: [ Endapo mtatofautiana katika jambo lolote basi lirejesheni kwa Allah na Mtume wake ikiwa ninyi mnamuamini Allah na siku ya mwisho, hilo ndilo jambo bora zaidi kwenu na marejeo mazuri zaidi ] Annisaa 59.**

**Na amesema Mtume swallallaahu alaihi wasallam: [ Ni juu yenu kushikamana na sunna zangu na sunna za makhalifa wangu waongofu wenye kuongoza, shikamaneni nazo ] Hadithi**

**sahihi ameipokea Ahmad.**

**SWALI LA KHAMSINI NA NNE: Namna gani tutampenda Allah na Mtume wake swallallahu alaihi wasallam?**

**JIBU: Tutawapenda kwa kuwatii na kufuata amri zao. Amesema Allah Mtukufu: [ Sema ikiwa ninyi mnampenda Allah basi nifuateni mimi , atakupendeni Allah na atakusameheni madhambi yenu, na Allah ni msamehevu na mwenye huruma ] Aali Imraan 31.**

**Na amesema Mtume swallallaahu alaihi wasallam: [ Hatokuwa mkamilifu wa Imani mmojawenu mpaka niwe napendwa zaidi kwake kuliko mzazi wake na mtoto wake na watu wote ] Bukhari na Muslim.**

**SWALI LA KHAMSINI NA TANO: Je, tuache kutenda mema na tubweteke katika makadirio ya Allah ?**

**JIBU: Hatutakiwi kuacha kutenda wema; kwa kauli ya Allah Mtukufu: [ Basi yeyote atakayetoa sadaka na akamcha Allah * Na akaamini malipo mema * Basi tutamfanyia wepesi katika njia za kheri ] Allail 5-7**

**Na kauli yake Mtume swallallaahu alaihi wasallam: [ Tendeni wema kwani kila mmoja amewepesishiwa katika yale ambayo ameumbiwa ] Ameipokea Bukhari na Muslim.**

**SUNNA NA BIDAA.**

**SWALI LA KHAMSINI NA SITA: Je, katika dini kuna bidaa nzuri?**

**JIBU: Hakuna katika dini bidaa nzuri, na dalili ni kauli yake Allah Mtukufu: [ Leo hii nimekukamilishieni dini yenu na nimetimiza juu yenu neema zangu na nimeridhia uislamu kuwa dini yenu ] Al-maaidah 3.**

**Na kauli yake Mtume swallallaahu alaihi wasallam: [ Na kila bidaa ni upotevu , na kila upotevu ni motoni ] Hadithi sahihi ameipokea Ahmad na wengineo.**

**SWALI LA KHAMSINI NA SABA: Ni ipi bidaa katika dini?**

**JIBU: Bidaa katika dini ni kuzidisha ndani yake au kupunguza. Amesema Allah Mtukufu akiwakemea washirikina juu ya bidaa zao: [ Au washirikina wana washirika ambao wana-**

**wawekea sheria katika dini, sheria ambayo hajairuhusu Allah ] Ashuuraa 21.**

**Na amesema Mtume swallallaahu alaihi wasallam: [ Yeyote atakayezusha ndani ya dini yetu hii jambo ambalo halipo, basi litarejeshwa ] Bukhari na Muslim. Yaani halitakubaliwa.**

**SWALI LA KHAMSINI NA NANE: Je, katika dini kuna mwenendo mzuri?**

**JIBU: Ndiyo; ndani ya uislamu kuna mwenendo mzuri. Na amesema Mtume swallallaahu alaihi wasallam [ Yeyote atakayeanzisha mwenendo mzuri katika Uislamu, basi atapata malipo yake na malipo ya watakaoufanyia kazi baada yake pasina kupunguziwa chochote katika malipo yake ] Ameipokea Bukhari.**

**SWALI LA KHAMSINI NA TISA: Lini watanusuriwa waislamu?**

**JIBU: Watanusuriwa waislamu pindi watakaporejea katika kufanyia kazi kitabu cha Mola wao na sunna za Mtume wao swallallaahu alaihi wasallam , na wakashikamana na kueneza Tauhidi na wakatahadharisha dhidi ya ushirikina kwa aina zake tofautitofauti zinazodhihiri na wakaandaa nguvu wanayoiweza dhidi ya maadui wao.**

**Amesema Allah Mtukufu: [ Enyi mlioamini endapo mtamtii Allah atakunusuruni na ataithibitisha miguu yenu ] Muhammad 7.**

**Na akasema pia : [ Allah amewaahidi wale walioamini miongoni mwenu atawatawalisha katika ardhi kama alivyowatawalisha wale waliokuwa kabla yao na ataiimarisha dini yao ambayo ameiridhia kwao na atawabadilishia amani baada ya hofu yao, waniabudu mimi wasinishirikishe na chochote ] Annuur 55.**

**DUA YENYE KUJIBIWA:**

**Amesema Mtume swallallaahu alaihi wasallam: [ Hatopatwa mja na majonzi na huzuni akasema : “ Ewe Allah hakika mimi ni mja wako, na mtoto wa mja wako, na mtoto wa mjakazi wako, utosi wangu upo katika mikono yako, hukumu yako ni yenye kunipitia, makadirio yako juu yangu ni ya uadilifu, nakuomba kwa kila jina lako ambalo umejiita kwalo mwenyewe au umeliteremsha ndani ya kitabu chako au umemfundisha yeyote katika viumbe wako, au umepwekeka nalo katika elimu yako ya ghaibu iliyopo kwako , nakuomba ujaalie Qur’an iwe chemchem ya moyo wangu , na nuru ya kifua changu na kifuniko cha huzuni yangu na yenye kuondosha majonzi yangu “ isipokuwa Allah atamuondoshea ma-**

**jonzi yake na huzuni yake na atambadilishia faraja katika nafasi ya huzuni na majonzi ] Hadithi Sahihi imepokelewa na Ahmad.**

## (Faida ya) ITIKADI HII:

**Mafikio ya muislamu katika utukufu au kuangamia yanategemea juu ya itikadi. Na hakika cha muhimu zaidi kilichomo ndani yake ni kumpwekesha Allah jambo ambalo Allah ulimwengu kwa ajili yake, na ametuma mitume ili kulihakiki. Huyu Mtume wa Allah swallallaahu alaihi wasallam alibakia katika mji wa Makka miaka kumi na tatu akitoa wito kuelekea katika kumpwekesha Allah katika kumuabudu na kumuomba yeye peke yake kinyume na mwingine: [ Na hakika misikiti yote ni ya Allah, basi msimuombe yeyote pamoja na Allah ] Al-jinn.**

**Na miongoni mwa kumpwekesha Allah ni kuamini sifa za Allah ; na miongoni mwazo ni : Allah kuwa juu ya arshi yake; ili kuhakiki kauli yake Allah Mtukufu : [ Allah mwingi wa rehma yupo juu ya arshi amestawi ] Twaha 5; yaani yupo juu.**

**Na kwamba, Allah aliyetakasika yupo pamoja na waja wake kwa usikivu wake na kuona kwake na elimu yake: [ Akasema Allah; msiogope hakika mimi nipo pamoja nanyi , nasikia na naona ] Twaaha 46.**

## MWISHO:

**Risala hii imeandaliwa kwa lugha ya Kiswahili ili kuwepesisha ufundishaji wa somo la Itikadi katika semina maalumu ya wanafunzi waliomaliza darasa la saba , iliyoanza tarehe 30/09/2023 mpaka 30/12/2023 ndani ya markaz Ibnu Uthaimin Hazina Dodoma.**

**Tunapokea nasaha zako:**

**0683 75 81 61**